

Kanisa Katoliki, Jimbo Kuu la Dar es Salaam

Parokia ya Mt. Martha, Mikocheni

HISTORIA YA PAROKIA

AGOSTI 2019

1.0 UTANGULIZI

Parokia ya Mtakatifu Martha Mikocheni ipo barabara ya Warioba, mita mia sita kutoka barabara ya Mwai Kibaki iliyokuwa ikijulikana kama Old Bagamoyo, kuelekea shule ya Laureate Mikocheni, na imepakana na ofisi za zamani za Taasisi ya Elimu Tanzania kwa upande wa mashariki na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa nyuma.

Eneo la Mikocheni lilianza kukaliwa na watu kwa wingi miaka ya 1980s na kufikia miaka ya 1990s, idadi ya wakazi wa Mikocheni iliongezeka sana. Kwa sababu ya kuongezeka kwa watu, haja ya kupata huduma mbalimbali za kijamii ilijitokeza mojawapo ya hizo ikiwa ni huduma za kiroho.

Kutokana na ukosefu wa huduma za kiroho katika eneo hilo, wakazi waanzilishi walijikuta kila mmoja akielekea alikozoea au alikoweza kufika kwa urahisi zaidi ili kujipatia huduma hiyo.

Baada ya kubainisha tatizo hili, waamini Wakatoliki waliamua kulitafutia ufumbuzi. Kwanza kabisa suala la msingi lilikuwa kujua eneo hilo lilikua chini ya Parokia ipi na kuainisha mipaka.

Mipaka iliyoainishwa ilionyesha kwamba eneo kutoka mto Kijitonyama hadi mto wa Mlalakuwa uliopo kaskazini magharibi lipo chini ya Parokia ya Mwenge. Wakazi wa eneo hili walitambuliwa rasmi na Parokia ya Mwenge na kuwa mojawapo ya kanda zilizounda Parokia ya Mwenge ikijulikata kwa jina la Kanda ya Mikocheni.

Viongozi wa kwanza wa Kanda hii walikua ni:-

1) Marina P. Mlunde - Mwenyekiti
2) Jacob Masimbuzi - Makamu Mwenyekiti
3) Ivor Ndumbati - Katibu

2.0 HUDUMA ZA IBADA

Huduma za ibada zilipatikana Parokiani Mwenge. Siku za Jumatano jioni kulikuwa na ibada maalumu kwa ajili ya watoto hasa wale wa mafundisho ya Komunyo ya kwanza na Kipaimara. Ilikua vigumu kwa watoto wa Mikocheni kuhudhuria ibada hiyo kwa sababu ya kuogopa kugongwa na magari wakati wakivuka barabara kuu ya Ali Hassan Mwinyi lakini pia njia walizokuwa wakitumia kwa wakati huo zilikuwa za vichochoro na za hatari.

Pd. Karol Szojda aliyekuwa Paroko wa Mwenge kipindi hicho na ambaye kwa sasa ni marehemu, aliona tatizo hilo hivyo akaamua kusoma ibada ya misa kwa ajili ya watoto hao kila Jumatano jioni katika mojawapo ya madarasa ya shule ya msingi Ushindi. Watu wazima wa Mikocheni walipojua kuwa kila Jumatano jioni kulikua na ibada ya watoto nao wakaanza kuhudhuria.

Umuhimu wa kusogeza ibada ya misa Jumapili karibu ulionekana pia kwa ajili ya watoto, wazee na wagonjwa. Uongozi wa kipindi hicho walipeleka maombi kwa mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu iliyoko Mikocheni na inayopakana na kanisa letu.

Mkurugenzi alitoa kibali cha mwaka mmoja, hivyo ibada ya misa ikawa inasomwa saa 11 jioni kila Jumapili. Baada ya mwaka mmoja yalifanyika mawasiliano ya mdomo kuomba huduma ziendelee. Huduma ya ibada ya Jumapili jioni iliendelea kutolewa hadi mapema 1995 ambapo ratiba ilibadilika na kuanza kutoa huduma ya misa asubuhi.

Huduma ya misa katika majengo ya Taasisi iliendelea hadi tarehe 18 Aprili 1999 na tarehe 25 Aprili, 1999 misa ya kwanza ilisomwa katika kanisa la muda lililojengwa katika eneo ilipo parokia sasa. Wakati huu kanisa hili lilijulikana kama Nyumba ya sala.

3.0 UTAFUTAJI KIWANJA

Utafutaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa la Mikocheni ulianza mapema mwaka 1994 ambapo barua ya kwanza ya maombi ilitumwa Halmashauri ya Jiji.

Hapo awali hatua za utafutaji kiwanja zilikuwa zikichukuliwa na waamini wa sehemu mbalimbali za Mikocheni A na B bila kuwasiliana. Hata hivyo ilipofika mwaka 1994, pande zote mbili za Mikocheni A na B wakishirikiana na Parokia ya Mwenge waliungana pamoja na kuweka msukumo mkubwa katika suala hili. Aidha mnamo Januari, 1995 jitihada za utafutaji kiwanja zilianza kupata mwelekeo mzuri baada ya kupata ramani ya eneo lililokuwa wazi jirani na Taasisi ya Elimu ambapo ndipo lilipo kanisa la sasa.

Suala la kiwanja halikuwa rahisi hata baada ya kuainisha eneo lililokuwa wazi. Kuna matatizo mengi yaliyojitokeza hasa huko wizarani na sehemu zinginezo.

Pamoja na yote hayo uongozi wa Kanda ya Mikocheni kwa kushirikiana na Parokia ulijizatiti vilivyo kulifuatilia suala hili hadi likafanikiwa.

Mwezi Januari 1998 barua ya kupewa kiwanja (Offer) ilipatikana na tarehe 26 Julai, 1998 Paroko Pd. Krystian alitangaza rasmi kupatikana kwa hati ya kumiliki ardhi ya Kiwanja cha Kanisa, hati Na. 47558 ya muda wa miaka 66. Ilikuwa ni furaha kubwa sana kwa waamini wa Mikocheni na Parokia ya Mwenge kwa ujumla kupata habari hizo.

4.0 UJENZI WA KANISA LA MUDA

Baada ya kupata hati, ujenzi wa kanisa la muda ulianza mapema 1999 sambamba na ujenzi wa uzio ili kulinda kiwanja chetu wakati ibada ikiendelea kufanyika katika majengo ya Taasisi ya Elimu. Tarehe 25 Aprili, 1999 misa ya kwanza ilisomwa katika kanisa la muda ambalo hata hivyo halikuwa limekamilika vizuri. Pd. Eugene C. Lyamtane wa jimbo la Moshi ambaye alikua mwanafunzi wa chuo kikuu cha Dar es Salaam, alisoma misa ya kwanza katika eneo la kanisa.



Kanisa la muda

Shughuli nyingine zilifanyika sambamba na ujenzi wa kanisa hili ambazo ni kuweka maji katika eneo la kiwanja, kujenga kibanda cha mlinzi, choo cha muda na vilevile tenki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 20,000 kwa ajili ya ujenzi uliokuwa unaendelea na wa hapo baadae.

Padri Jude Massawe ambaye alipokea uongozi wa Parokia ya Mwenge kutoka kwa Pd. Krystian hapo mwaka 1999, ndiye aliyekuwa mstari wa mbele katika kusimamia shughuli mbalimbali za ujenzi.

Baada ya kanisa la muda kukamilika mwishoni mwa mwaka 1999 tulitangazwa rasmi kuwa kigango cha Mt. Martha Mikocheni.

Viongozi wa kwanza wa Kigango walikuwa ni:-

Mzee Henri J. Msuya (RIP)	-	Mwenyekiti
Bibi Bernadette Sebastian	-	Makamu Mwenyekiti
Bw. Severin Mbuya (RIP)	-	Katibu
Bw.Fred Kitangwa	-	Katibu Msaidizi
Bw. Joseph Mushumbusi (RIP)	-	Mwekahazina

Padri Jude Massawe aliunda kamati ya Ujenzi akiwashirikisha wajumbe hao hapo juu pamoja na Mama Edwina Lupembe ambaye alikuwa Mwenyekiti, Mama Sara Nyoni na mtaalamu Joseph Kavishe. Kamati hii ilihusika na mambo yote ya ujenzi wa Kanisa.

5.0 UJENZI WA KANISA LA KUDUMU

Mnamo tarehe 28 Julai 2002, sikukuu ya Mtakatifu Martha, uwanja wa kujenga Kanisa la kudumu ulibarikiwa rasmi na Mwadhama Emmanuel Kardinali Wamala kutoka Jimbo Kuu la Kampala Uganda ambaye alikuwa amekuja kwenye mkutano wa AMECEA na alifika Mikocheni akiwa anaongozana na Mhashamu Askofu Nestory Timanywa wa Jimbo la Bukoba.



Mwadhama Emmanuel Kardinali Wamala
Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Kampala akisalimiana na Waamini wa Mikocheni

Baada ya kiwanja kubarikiwa ujenzi ulianza kwa nguvu zote. Wakati ujenzi wa Kanisa unaendelea, mwezi Agosti, 2005 tulianza pia ujenzi wa nyumba ya Mapadri baada ya kugundua kuwa tusingeweza kuwa Parokia bila kuwa na nyumba ya Mapadri. Ilipofika Desemba, 2006 nyumba ya Mapadri ilifikia kiwango ambacho kiliwezesha Mapadri kuishi ndani bila taabu yoyote. Baada ya kufikia hatua hiyo, Septemba, 2006 tulianza kujenga choo cha kisasa cha Parokia ambacho kilikamilika na kuzinduliwa na Mhashamu Askofu Methodius Kilaini tarehe 15 April, 2007.



Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo baada ya kukagua ujenzi wa nyumba ya Mapadri.

Tarehe 24 Juni, 2006 Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo alitutangaza rasmi kuwa Parokia alipokuja kutoa Sakramenti ya Kipaimara kwa watoto wa Parokia. Tuliendelea kupata huduma kutoka kwa Paroko wa Mwenge hadi tarehe 24 Desemba 2006 tulipompata Paroko wetu wa kwanza Padri Joseph Massenge.

Padri Joseph Massenge ndiye aliyeanzisha utaratibu wa kubariki nyumba zote za wanaparokia hapa Parokiani kipindi cha Pasaka, utaratibu ambao unaendelea hadi sasa. Kwa utaratibu huu, Padri akishafika kwenye nyumba ya kwanza na kuibariki, wanajumuiya wanaungana naye kwenda kubariki nyumba zingine zinazofuatia na zoezi hili linaendelea mpaka kwenye nyumba ya mwisho ambapo huadhimisha misa ya pamoja ya wanajumuiya wote.

Viongozi wa kwanza wa Halmashauri Walei Parokia walikua ni:-

Bwana P.J. Sebastian	-	Mwenyekiti
Bwana Fred Kitangwa	-	Makamu Mwenyekiti
Bwana Severin Mbuya (RIP)	-	Katibu
Bibi Felicia Ochola	-	Katibu Msaidizi
Bwana Joseph Mushumbusi (RIP)	-	Mweka Hazina

Tarehe 29 June, 2008 Kanisa letu lilibarikiwa rasmi na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo na mwaka huo huo Padri Massenge alikwenda masomoni huko Roma hivyo tukampata Paroko mwingine Padri Audax Kaasa.



Kanisa baada ya kukamilika



Nyumba ya Mapadre baada ya kukamilika




Choo cha Parokia baada ya kukamilika

6.0 ENEO LINALOUNDA PAROKIA YA MT. MARTHA MIKOCHENI

Kutokana na ramani inayoonyesha mipaka ya parokia kanisa Katoliki Dekania ya Mt. Petro, mipaka ya Parokia ya Mikocheni kwa upande wa Kaskazini ni mto Mlalakuwa unaotokea daraja lililopo SUMA JKT Mwenge kupitia daraja la JKT Mlalakuwa mpaka baharí ya Hindi na kwa upande wa Kusini ni mto Kijitonyama unaotokea Oilcom Sayansi kupitia daraja lililopo shule ya chekechea Feza mpaka baharí ya Hindi. Upande wa Mashariki ni baharí ya Hindi na upande wa Magharibi ni barabara ya Bagamoyo.

Ndani ya eneo la Parokia ndipo kilipo kituo cha Redio Maria, nyumba ya Passionist Fathers, ofisi za CEFA na nyumba ya Masista wa Mt. Teresia wa Mtoto Yesu.



Ramani inayoonyesha mipaka ya Parokia ya Mt. Martha Mikocheni

7.0 MAPADRE NA WATAWA WALIOFANYA KAZI MIKOCHENI

7.1 Mapadre waliotupatia huduma

Tangu mwanzo tulipoanza harakati za kutafuta mahali pa kufanyia ibada ya misa takatifu na kabla ya kuwa Parokia, tulikuwa tukipata huduma toka kwa Maparoko wa Mwenge wafuatao:-

1) Pd. Karol Szojda
2) Pd. Mathias Millanzi
3) Pd. James Aloys Weyker
4) Pd. Mieczyslaw Kijaczek
5) Pd. Krystian Golisz
6) Pd. Jude Massawe
7) Pd. Christopher Luoga

Hatuwezi kumsahau Pd. Gleason Carl aliyejulikana pia kwa jina la Pd. Babu na ambaye alikuwa Paroko msaidizi Mwenge kwa vipindi vitatu tofauti, yaani 1988 - 1991; 1993 – 1995 na 1997 - 2006 alipohamishwa. Padri huyu alikuwa mstari wa mbele kutoa huduma za misa hapa Mikocheni na kutembelea wagonjwa na wazee wasiojiweza. Mara nyingi alitembea kwa miguu kutoka Mwenge hadi Mikocheni akiwa amevaa kofia yake kubwa ya kujikinga na jua kali la Dar es Salaam. Padri huyu aliyezaliwa mwaka 1928, alifariki huko Marekani (USA) mwaka 2018. Mungu azikumbuke kazi alizozifanya na amjalie pumziko la amani. Tunawakumbuka pia Pd. Stanislaus Goral na marehemu Pd. Marian Hayzyk waliokuwa pia Maparoko wasaidizi Mwenge kwa huduma walizotupatia.

Baada ya kuwa Parokia, mapadri waliofanya kazi katika Parokia yetu kwa mfuatano ni kama ifuatavyo:-

Kipindi	Paroko	Paroko Msaidizi
24.12.2006 – 04.07.2008	Pd Joseph Massenge	-
05.07.2008 – 26.05.2012	Pd Audax Kaasa	Pd. Paul Haule (Julai, 2008 - Januari, 2009)
		Pd. Andrew Mwekibindu (2009 – 2010)
		Pd. Ladislaus Kapinda (Jan, 2012 - Oct, 2012)
27.05.2012 –19.07.2015	Pd Vitalis James Kassembo	Pd. Gilbert Makuru (14 Dec,2012 – 6 Jan, 2015)
20.07.2015 – 13.01.2019	Pd Andrew Mwekibindu	Pd. Ladislaus Kapinda (Julai, 2015 – Julai, 2016)
19.01.2019 – mpaka sasa	Pd Asis Mendonça	-

Kuna Mapadri wawili waliofanya kazi kwa kukaimu kwa kipindi kifupi kuanzia tarehe 14 Januari 2019 hadi 18 Januari 2019 baada ya kutokea kifo cha Pd. Andrew Mwekibindu kwakuwa tulikuwa hatuna Paroko Msaidizi. Mapadri hao ni Pd. Nicolaus Masamba aliyekaimu Uparoko na Pd. Ernest Boyo aliyekaimu Uparoko Msaidizi.

Wapo pia Mapadri wasiokuwa wa Jimbo letu lakini walifanya kazi kwenye Parokia yetu wakati wa masomo yao kwenye vyuo vikuu mbalimbali hapa Dar es Salaam. Mapadri hao ni Pd. Eliazar Petro Mamilo wa Jimbo la Kigoma aliyekuwa akisoma Chuo Kikuu Ardhi na ambaye alifika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2007 na alihamishiwa Kanisa Kuu la Mt. Yosefu Julai, 2008. Padre wa pili ni Pd. Pantaleo Rutambuka wa Jimbo la Kayanga, Karagwe ambaye alifika Julai, 2010 na kuondoka Novemba, 2011. Padre wa tatu ni Pd. Gideon Rwezahura wa Jimbo la Bukoba aliyekuwa akisoma shule ya Sheria na ambaye alifika tarehe 15/08/2017 na kuondoka tarehe 08/08/2018.

Mapadre wetu hawa wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii na kujituma bila kujibakiza. Kwa kipindi chote toka Mikocheni iwe Parokia tumekumbana na changamoto mbalimbali. Japo changamoto ni sehemu ya maisha, zipo changamoto mbili ambazo ni vigumu kuzisahau.

Changamoto ya kwanza ni kutokea kwa tukio la wizi hapa Parokiani tarehe 22/05/2012 ambapo wezi waliokuwa na silaha waliingia Parokiani na kuwakamata, kuwafunga na kuwaumiza walinzi wawili kati ya watatu waliokuwa kwenye lindo. Wezi hao walifanya uharibifu mkubwa wa mali na kuiba vitu mbalimbali likiwepo gari ambalo baadaye lilipatikana likiwa limetelekezwa. Tukio hilo pia lilisababisha Padri Audax Kaasa aliyekuwa Paroko wetu kuvunjika miguu yote miwili na ikabidi kupelekwa India kwa matibabu. Tunamshukuru Mungu miguu yake ilipona vizuri na sasa ni vigumu kutambua kama aliwahi kuvunjika miguu yote miwili.

Changamoto ya pili ni kifo cha Pd. Andrew Mwekibindu aliyekuwa Paroko wa Mikocheni kuanzia tarehe 20/07/2015 hadi alipofariki usiku wa kuamkia tarehe 13/01/2019. Paroko

huyu alitupenda sana na alitufundisha kufuata taratibu za kanisa bila kupinda. Tunazidi kumuombea kwa Mungu ili ampumzishe kwenye Ufalme wake wa amani.

7.2 Masista Waliohudumu Parokia ya Mikocheni

Parokia ya Mikocheni imekuwa ikihudumiwa na Masista wa Shirika la Teresia wa Mtoto Yesu, wanaojulikana kama Wateresina, ambalo makao yake makuu yapo Iringa. Masista hao wanayo nyumba yao eneo la Mikocheni. Toka kuanzishwa kwa Parokia mpaka sasa, Masista wafuatao wamehudumu katika Parokia ya Mikocheni:-

Kipindi	Jina la Sista
2003 – 2006	Sr. Petronila Magola
2004 - 2010	Sr. Rustica Lungu
2008 - 2013	Sr. Neema Changa
2013 – 2014	Sr. Frida Mdemu
2014 – sasa	Sr. Lucy G. Mgata
2017 - sasa	Sr. Emmanuala Mkonda

8.0 VIONGOZI WA HALMASHAURI WALEI PAROKIA

Viongozi wa Halmashauri ya Walei ngazi ya Parokia tokea kuanzishwa kwa Parokia ni kama ifuatavyo:-

Kipindi	Jina	Nafasi
2006 – 2009	Pantaleo J. Sebastian	Mwenyekiti
	Fred Kitangwa	Makamu Mwenyekiti
	Severin Mbuya (RIP)/DrNicholas Mlingi	Katibu
	Felicia Ochola	Katibu Msaidizi
	Joseph Mushumbusi (RIP)	Mwekahazina
2010 – 2012	Pantaleo J. Sebastian	Mwenyekiti
	Fred Kitangwa	Makamu Mwenyekiti
	Sixtus Basil Kessy	Katibu
	Alex P. Matoke	Katibu Msaidizi
	Concesa Shayo (RIP)	Mwekahazina
2013 – 2015	Pantaleo J. Sebastian	Mwenyekiti
	Dafroza Tairo	Makamu Mwenyekiti
	Sixtus Basil Kessy	Katibu
	Grayson Edward	Katibu Msaidizi
	Concesa Shayo (RIP)	Mwekahazina
2016 – 2019	Sixtus Basil Kessy	Mwenyekiti
	Dafroza Tairo	Makamu Mwenyekiti
	Alex P. Matoke	Katibu
	Grayson Edward/Mwilu Kibassa	Katibu Msaidizi
	Bariki Keenja	Mwekahazina



Paroko Pd. Asis Mendonça na Mwenyekiti wa Halmashauri Walei Ndg. Sixtus Kessy wakipanda mti wa kumbukumbu ya Jubilei ya Miaka 50 ya Halmashauri Walei Tanzania tarehe9 Juni, 2019Sikukuu ya Pentekoste

9.0 KAMATI MBALIMBALI

Parokia ya Mikocheni ina kamati tano za kikatiba na kamati nane za kitaaluma. Kamati za kikatiba ni kamati ya Malezi na Familia, kamati ya Ibada na Liturjia, kamati ya Haki na Amani, kamati ya Elimu ya Dini, Mafundisho ya Kanisa na Teolojia na kamati ya Uchumi na Fedha.

Kamati za kitaaluma ni kamati ya Ujenzi, kamati ya Sheria, kamati ya Ulinzi na Usalama, kamati ya Afya, kamati ya Usafi na Mazingira, kamati ya “Fund Raising”, kamati ya Tafrija na Sherehe, na kamati ya Michezo na Burudani.

Kamati hizi kwa kushirikiana na kamati Tendaji ya Parokia hutimiza majukumu yao mbalimbali na hufanya kazi kwa kuhakikisha kuwa mipango na shughuli mbalimbali za Parokia zinafanywa kwa tija na ufanisi mkubwa.

10.0 JUMUIYA NDOGONDOGO ZA KIKRISTU (JNNK)

Parokia ya Mikocheni ina Jumla ya Kanda 4 na Jumuiya 21 kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini. Idadi ya Wakristu hubadilika mara kwa mara ila kulingana na sensa iliyofanyika mwaka 2016 Parokia ya Mikocheni ina Waamini 1,275.

Kanda	Jumuiya	Idadi ya Jumuiya
Mt. Mathayo 'A'	Mt. Bernadine	6
	Mt. Maria Magdalena	
	Mt. Maxmillian Maria Kolbe	
	Mt. Petro Mtume	
	Mt. Augustino	
	Mt. Yuda Thadei	
Mt. Marko 'B'	Mt. Vincent Ferrer	4
	Mt. Papa Leo IX	
	Wat. Mashahidi wa Uganda	
	Mt. Maria Goretti	
Mt. Luka USHINDI	Mt. Petro Kristologi	5
	Mt. Rafael	
	Mt. Inyasi wa Loyola	
	Mt. Anna	
	Mt. Martha	
Mt. Yohane STAMICO	Mt. Yoseph Mfanyakazi	6
	Mt. Mathias Mtume	
	Mt. Josephine Bakhita	
	Mt. Antoni wa Padua	
	Mt. Monica	
	Mt. Yuda Thadei	
Jumla		**21**

11.0 VYAMA VYA KITUME (VMJ)

Baada ya Ibada za misa kuanza kufanyika Mikocheni umuhimu wa kuwa na kwaya ulijitokeza. Hivyo kwaya ya Mt. Teresia wa Mtoto Yesu ilianza rasmi mwezi Juni, 1995 na wanakwaya waanzilishi walikuwa kumi na moja na walimu wawili mmoja wao alikuwa akitoka Mburahati. Mwalimu toka Mburahati alifundisha kwaya hiyo kwa muda na baada ya kwaya kupata mwalimu mwingine huyo aliacha. Kwaya iliendelea kuimarika siku hadi siku na baadhi wa Waamini walikuwa wakijitolea misaada mbalimbali mfano unununzi wa sare za kwaya, unununzi wa vifaa kama vile ngoma, kayamba n.k. Aidha Paroko Pd. Krystian Golisz, alitoa kinanda. Kwaya iliendelea kukua hadi kufikia idadi ya wanakwaya 20 wakiwa pia na walimu wa kwaya.

Baada ya Mikocheni kutangazwa kuwa Parokia, ziliundwa kwaya nyingine mbili na kufanya jumla ya kwaya kuwa tatu ambazo ni kwaya za Mt. Theresia wa Mtoto Yesu, Mt. Josephine Bakhita, na Mt. Yuda Thadei. Watoto nao wana kwaya yao ambayo huimba kwenye misa zao na wakati mwingine kwenye misa za wakubwa kama wakialikwa.

Pamoja na kwaya, mpaka sasa Parokia ya Mikocheni ina jumla ya vyama vya Kitume nane, ikiwa Vyama visivyo vya hiari ni vinne ambavyo ni Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), Utume wa Wanaume Katoliki (UWAKA), Umoja wa Vijana na Utoto Mtakatifu. Aidha Vyama vya hiari navyo ni vinne ambavyo ni Moyo Mtakatifu wa Yesu, Legio Maria, Karismatiki Katoliki na UKWAKATA.

Kwa sasa Parokia ipo kwenye mchakato wa kuanzisha vyama vingine viwili ambavyo ni Wazee na Wastaafu pamoja na Skauti Katoliki.



Utoto Mtakatifu



UKWAKWATA

12.0 MIPANGO YA MAENDELEO

Kwa sasa Parokia ya Mikocheni imeelekeza nguvu zake zote katika kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa Parokia ambao umekwisha ezekwa na kazi za 'finishes' zinaendelea. Ukumbi huu ulioanza kujengwa tarehe 9 Machi, 2012 baada ya kiwanja kubarikiwa na Baba Kardinali, ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuchukua watu 510 waliokaa pamoja na meza. Sambamba na jukumu hilo, Parokia inaweka 'pavers' kwenye eneo la kanisa ili kuondokana na changamoto ya vumbi, tope na maji. Baada ya kazi hizo, Parokia itajenga Grotto ya Bikira Maria.



Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo akibariki uwanja kwa ajili ya kuanza kujenga ukumbi wa Parokia



Ukumbi wa Parokia ukiwa kwenye hatua za mwisho za ujenzi

13.0 HITIMISHO

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuilinda Parokia yetu tangu ilipoanzishwa mpaka sasa. Kwa maombezi ya Mt. Martha msimamizi wa Parokia yetu, Mungu azidi kuilinda Parokia yetu na kuwajalia mapadri, masista na waamini wote afya ya roho na ya mwili. Aidha tunawashukuru Mapadri kwa huduma mbalimbali za kiroho wanazotupatia na Masista kwa kuhudumu katika Parokia yetu. Tunawashukuru pia ndugu zetu waamini kwa kushiriki kwao katika shughuli mbalimbali za kujenga Parokia yetu. Tunawaomba waamini wote, kwa kushirikiana na uongozi wa Parokia, kujitahidi kupunguza kama si kumaliza changamoto mbalimbali zinazoikabili Parokia yetu. Mungu atupe amani yake na kutujalia furaha, afya na neema tele, Amina.